# Bajeti 2024: Haki Na Usawa Kwa Kila Kizazi

April 16, 2024 | Ottawa, Ontario | Idara Ya Fedha Ya Canada

Leo, Mheshimiwa Chrystia Freeland, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Fedha, ametoa Bajeti ya 2024: Haki na Usawa kwa Kila Kizazi.

Ni mpango wa kujenga Canada ambayo inafanya kazi vizuri na kunufaisha kila kizazi, ambapo vizazi vya vijana vinaweza kusonga mbele, ambapo juhudi zao zinalipa, na ambapo wanaweza kununua au kukodisha nyumba zao wenyewe—ambapo kila mtu ana nafasi na haki ya kuwa na maisha bora ya tabaka la kati.

**Kwanza, Bajeti ya 2024 inachukua hatua za madhubuti kujenga nyumba zaidi.** Kwa sababu njia bora zaidi ya kufanya bei za nyumba na kodi kuwa nafuu zaidi ni kuongeza upatikanaji—na kwa haraka. Bajeti ya 2024 inaainisha mkakati wa kufungua au kujenga nyumba mpya milioni 3.87 ifikapo mwaka 2031. Hatua muhimu zinajumuisha kuzindua *Mpango Mpya wa Ardhi za Umma kwa Ajili ya Nyumba* na Mfuko Mpya wa Udhibiti wa Nyumba za Kukodisha wa Canada, kuimarisha Mkataba wa Mikopo ya Nyumba wa Canada, na kuunda Hati Mpya Za Haki za Wapangaji nchini Canada.

**Pili, Bajeti ya 2024 itasaidia kupunguza gharama za maisha**. Kwa kujenga juu ya upanuzi wa kipekee wa mtandao wa usalama wa jamii wa Canada—kutoka huduma ya watoto kwa dola 10 kwa siku, hadi huduma ya meno kwa raia au wakazi wa Canada wasio na bima, hadi awamu ya kwanza ya huduma ya afya ya dawa kwa wote—Bajeti ya 2024 inaendeleza kazi na mkakati wa serikali wa kupunguza gharama za kila siku kwa raia na wakazi wa Canada. Hii inajumuisha kusaidia kudhibiti mfumuko wa gharama za vyakula, kupambana na ada za ukopaji zisizo za lazima ili kufanya bei kuwa za haki zaidi, na kupunguza gharama za huduma za benki. Bajeti ya 2024 inafanya uwekezaji mpya wa kubadilisha mambo, ikiwa ni pamoja na uzinduzi wa Mpango Mpya wa Chakula Mashuleni wa Taifa na Fidia Mpya Kwa Watu Wenye Ulemavu nchini Canada.

**Tatu, Bajeti ya 2024 itakuza uchumi katika namna ambayo itashirikisha na kunufaisha watu wote**. Ni mpango utakaovutia na kuongeza uwekezaji, kuimarisha tija, na kuhamasisha aina za uvumbuzi ambazo zitaunda ajira nzuri zenye maana na kuifanya Canada kuwa mbele kiuchumi. Pia itatoa aina mpya za misaada ili kuwawezesha wajasiriamali na wabunifu bora zaidi kuwekeza mawazo na ubunifu wao hapa nchini Canada. Hii inajumuisha kuvutia uwekezaji zaidi katika uchumi unaozingatia mazingira ya tabia nchi kwa kupanua na kutoa mikopo mikubwa itokanayo na kodi na uwekezaji wa kiuchumi, kuhakikisha Canada inakuwa kiongozi katika matumizi ya akili bandia, na kuwekeza katika ruzuku za utafiti zilizoimarishwa ambazo zitatoa ajira nzuri na fursa mpya kwa vizazi vijana. Na hii inamaanisha kuhakikisha kuwa Watu wa Asili wanashiriki katika ukuaji huu kwa njia inayofaa kwao. Bajeti ya 2024 itafanya mfumo

wa kodi wa Canada kuwa wa haki zaidi unaowataka matajiri kulipa kodi sawa na kipato chao-ili tuweze kufanya uwekezaji utakaonufaisha na kustawisha kila kizazi, na kwa sababu sio sawa au haki kurithisha kizazi kijacho madeni kwa kutozingatia au kupuuza vigezo vyetu vya fedha. Bajeti ya 2024 ni mpango wa kiuchumi unaowajibika na wenye kuunga mkono malengo ya kifedha yaliyoanishwa kwenye *Taarifa ya Uchumi ya Vuli ya 2023*, unayoiona Canada ikiendelea kuwa na viwango vya chini vya upungufu wa deni na viwango vya Pato la Taifa miongoni mwa mataifa ya G7.

## Nukuu

"Serikali yetu ilipoingia madarakani kwa mara ya kwanza, iliahidi kuimarisha na kupanua tabaka la kati. Tumetimiza ahadi hiyo kwa kupunguza umaskini, hasa kwa watoto na wazee, na kwa kuunda mamilioni ya ajira nzuri kwa raia na wakazi wa Canada. Kazi yetu bado haijakamilika. Bajeti ya 2024 inafufua mkazo wetu wa kufungua mlango wa kuingia katika tabaka la kati kwa mamilioni ya wakazi na raia wa Canada vijana. Tutajenga nyumba zaidi na kusaidia kupunguza gharama za maisha. Tutaelekeza uchumi wetu kuelekea ukuaji unaoinua kila mtu. Hiyo ndio haki na usawa kwa kila kizazi."

*Mheshimiwa Chrystia Freeland, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Fedha*

## Nyaraka Zinazohusiana

Bajeti 2024: Haki na Usawa kwa Kila Kizazi
Bajeti 2024: Hotuba na Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Fedha
Bajeti 2024: Hatua Muhimu (zinapatikana katika lugha zisizo rasmi)
Maelezo ya Nyuma: Nyumba Nafuu Zaidi
Maelezo ya Nyuma: Mtandao Imara Zaidi wa Usalama wa Jamii
Maelezo ya Nyuma: Haki kwa Vizazi Vijana
Maelezo ya Nyuma: Ukuaji wa Uchumi na Uzalishaji
Maelezo ya Nyuma: Kuendeleza Biashara Ndogo
Maelezo ya Nyuma: Jamii Salama, Zenye Afya Zaidi
Maelezo ya Nyuma: Mustakabali wa Haki kwa Watu wa Asili
Maelezo ya Nyuma: Haki ya Kodi kwa Kila Kizazi
Bajeti 2024: Mfumo wa Benki Unaomlenga Mtumiaji nchini Canada

## Mawasiliano

### Vyombo Vya Habari Vinaweza Kuwasiliana Na;

Katherine Cuplinskas
Katibu wa Vyombo vya Habari na Mshauri Mkuu wa Mawasiliano
Ofisi ya Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Fedha
Katherine.Cuplinskas@fin.gc.ca

Mahusiano ya Vyombo vya Habari
Idara ya Fedha ya Canada
mediare@fin.gc.ca
613-369-4000

**Maswali au Maulizo ya Jumla**
Simu: 1-833-712-2292
TTY: 613-369-3230
Barua Pepe: financepublic-financepublique@fin.gc.ca